
# WANATAPATAPA OVYO

By: Martin Z. Yohana
Mererani 2006







*NB: Usiongeze wala kupunguza chochote ktk wimbo huu.*
*Usinakili wala kuutumia kibiashara (recording) pasipo idhini ya mtunzi.*
*zingatia hayo ili uepuke kusumbuliwa.*
*Simu: 0741-183 057*
*0746-952 019*

1. Hawa ndio wale wanaotapatapa ovyo, ndio wale wasiomtumaini Mungu
   Kila siku ni kiguu na njia eti wasaka pesa, hata kukumbuka kusali hawataki,
   Wamesahau ya kwamba Mwenyezi ndiye mtoa vyote, na ndiye mpaji wa vyote kwa wajawe.

2. Hawa ndio wale wanaomkufuru Mungu, ndio wanaochezea jina lake Mungu
   Wanaishi maisha ya uzinzi pasipo kufunga ndoa, na maisha yao hujaa machungu mengi
   Wengine wanaharibu miili eti wawe warembo, kana kwamba Mungu hakuwaubma vizuri.

3. Hawa ndio wale wanaomdhihaki Mungu, ndio wale wasioheshimu uhai wao
   Wanatumia vibaya miili yao kwa ukahaba, eti ili wajipatie kitu kidogo
   Wengine wanatelekeza ndoa sababu ya nyumba ndogo, na kuziacha familia zikiteseka.

4. Hawa ndio wale wanaompendeza Mungu, ndio wale wanaoshika njia zake Mungu
   Ndio waliyoyatoa maisha yao kuwa sadaka, kwa kumtumikia Mungu kwa uchaji.
   Wanaothamini uhai wao pia na majirani zao, wakisaidiana vema na kupendana.

***Copied By: G.M.Kombo***